

## **Learning by Ear – Illiteracy**

### **“A GIRL FINISHING SCHOOL”**

**Episode 01:**     “SIKU INAYOTATIZA ”

**Author:**           Frédéric GAKPARA

**Editor:**           Yann Durand

**Translator:**       Anne Thomas

- Characters:**
- PAPA WALI** (*Baba wa watoto watatu, mwenye umri wa miaka 52 – Mtoto wake wa kwanza wa kiume anaitwa Elinam, kisha anafuatwa na binti aitwaye Latifa na mwisho mtoto wa kiume aitwaye Jaurès. Anashughulika na karakana ya vyuma lakini hajui kusoma na kuandika. Biashara inamwendea vibaya kila kukicha kwa kuwa hajamudu kujifunza mbinu mpya za ufundii hivi kwamba hamudu ushindani mpya wa kibashara.*)
  - EPIPHANE** (*Mvulana wa umri wa miaka 18, ameajiriwa na Papa Wali. Ni mwerevu sana lakini hawezi kusoma wala kuandika kwa kuwa hakupata fursa ya kujinga na shule. Kadiri anavyopata shida kutoka na hali yake hiyo ya kutojua kusoma, ndivyo hamu yake ya kujua kusoma na kuandika inavyozidi.*)
  - MR TÔ** (*Mwenye umri wa miaka 38. Amesoma na ni mteja wa Papa Wali.*)
  - MAMOUA** (*Mwenye umri wa 39, mke na mama ya watoto wa Papa Wali. Ni mjamzito wa mtoto wao wa nne. Hajui kusoma na kuandika. Anafanya biashara ndogo ya kuuza uji wa unga wa mahindi mbele ya nyumba yao.*)
  - LATIFA** (*Ana umri wa miaka 15. Ni binti yao Papa Wali and Mamoua. Mwaka wa tisa huu anaosoma. Ni mwerevu kiasi*)

*kwamba hajawahi kurudia darasa lolote. Hata hivyo anakabiliwa na tatizo la wazazi wake kutaka kumwachisha masomo.)*

## INTRO

**Hujambo msikilizaji na karibu kwenye mfululizo mpya wa vipindi vyatya Noa Bongo Jenga Maisha Yako. Makala haya ya "Msichana anayemaliza masomo" yanaelezea masuala ya elimu na kutojua kusoma na kuandika. Utavisikia visa vyatya ndugu wawili latifa na Elinam, familia na marafiki wao katika vipindi kumi vifuatavyo.**

*Papa Wali ana umri wa miaka 52 aliyena watoto watatu ni msimamzi wa karakana ndogo ya kufua vyuma katika mji mmoja mdogo. Hajui kusoma na kuandika na hilo linaitatiza biashara yake kwasababu washindani wake ambao ni wachanga wana ufahamu mzuri zadi wa teknolojia za kisasa. Daftari lake la wateja wanaoagizia bidhaa limekuwa tupu kwamuda sasa. Familia yake nayo imetatizwa na hali mbaya ya bishara. Papa Wali ameitelekeza nyumba yake inayozidi kuwa hali mbaya kila kukicha. Hali katika karakakana hiyo ni mbaya leo hii. Papa Wali anatiwa wasiwasi na bili kubwa ya umeme walioipokea. Hasira za Papa Wali zote zinamuangukia mfanyakazi wake Epiphanie aliye na umri wa miaka 18 hivi ambaye pia hajui kusoma na kuandika."Siku inayotatiza' ndiyo makala ya kwanza ya mchezo huu.*

## **Scene 1, IN PAPA WALI'S WORKSHOP**

Papa Wali and Epiphane

**1. ATMO:**      **NOISE OF A WELDING MACHINE,  
HAMMERING ON A SHEET OF METAL.**

**2. PAPA WALI:** (**Very angry**) Sielewi kwa nini gharama ya umeme imepanda kiasi hiki. Katika karakana hii tuna mashine moja ya kuchomelea vyuma na nyingine ya kunoa. Epiphane! Kuna mawili tu ama unatumia umeme kwa njia nyingine ambazo sizijui au shirika la umeme linalighai...

**3. EPIPHANE:**      (**Very surprised**) Hapana mzee! La hasha!  
Sijawahi kutumia umeme kwa njia nyingine isiyoeleweka.

**4. PAPA WALI:** Hilo ndilo jibu lako? Kwanini gharama ya umeme imepanda kiasi hiki ilhali wateja ni wachache? Sijui kusoma na kuandika ila si mjinga!

**5. EPIPHANE:**      Mzee, hatuwezi kulalamika?

**6. PAPA WALI:** Tumlalamikie nani? Wezi wanaoiongoza nchi hii?  
Wao ndio wanaotunga sheria zinazowafaa wao na daima hawafanyi kosa. Wale wasiojua kusoma na kuandika ndio walio matatani zaidi.

**7. EPIPHANE:**      Kweli mzee. Lau ningekuwa nimesoma  
ningewapa kweli yangu...

**8. PAPA WALI:** Fyata mdomo wako! Ilikuwaje hata ukakosa kusoma, Epiphane? Tulipokuwa wadogo hatukuwa na namna kwa kuwa shule moja iliyokuwepo ilikuwa mbali. Lakini hali si hivyo kwako.

**9. EPIPHANE:** Mzee, unajua vizuri kwamba siwajui wazazi wangu wala sikuwa na mtu wa kunisomesha.

**10. PAPA WALI:** Hata hivyo mshukuru Mungu: Angalau una kazi! Kuna watu waliosoma lakini hawana chochote.

**11. SFX:** **NOISE OF A CAR ARRIVING AND PARKING IN FRONT OF THE WORKSHOP.**

**12. EPIPHANE:** Yule bwana wa taa amefika, mzee.

**13. PAPA WALI:** Zitoe taa nje!

**Scene 2, IN PAPA WALI'S WORKSHOP:**

Papa Wali, Epiphane and Mr Tô

**14. SFX ATMO: SOUND OF A GATE OPENING AND CLOSING. THE WELDING AND HAMMERING SOUNDS STOP. SOUND OF STEPS.**

**15. PAPA WALI:** (Loudly to Mr Tô who is arriving) Karibu  
Bwana Tô!

**16. MR TÔ:** (Talking as he approaches) Asante! U hali gani Papa  
Wali?

**17. PAPA WALI:** Twamshukuru Mungu. Tumejaliwa afya njema.  
Hivi hapa vitu ulivyoagiza, Bwana Tô.

**18. SFX: SOUND OF SEVERAL GARDEN LAMPS BEING DRAGGED ON THE FLOOR**

**19. MR TÔ:** Usiniambie kwamba hizi ndizo taa zangu!

**20. PAPA WALI:** Kuna shida gani, Bwana Tô?

**21. MR TÔ:** Shida? Hivi mnanichezea nini? Waona kwamba hizi taa  
ndizo zinazofaa kwenye bustani yangu?

**22. PAPA WALI:** Lakini Bwana Tô, hizi taa ndizo ulizoagiza au  
sizo?

**23. MR TÔ:** Aka! Hivi vipande vyatya chuma vilivyopinda?

Nilikuonyesha sampuli zilizotengenezwa na kakangu ama sivyo? Je hizi ndizo nilizokuonyesha? (**Pause, annoyed**) Afadhali ningekuwa nimemuagiza yule aliyemtengenezea kakangu! Itakuwaje mtu mwenye uzoefu wa siku nyingi kama wewe kufanya kazi mbaya jinsi hii?

**24. PAPA WALI:** Tatizo letu ni kwamba tunatengeneza kila kitu chetu kwa mikono. Katu huwezi kuifananisha kazi yetu na ile iliyotengenezwa kwa mashine...

**25. MR TÔ:** Kwa nini hamna vifaa sawa na karakana nyingine za vyuma. (**scornfully**) Hatumo tena katika karne ya zama za mababu zetu!

**26. PAPA WALI:** Mashine ni ghali na hapa nilipo nashindwa kumlipa mfanyakazi wangu...

**27. MR TÔ:** Afadhali hivyo kama kutengeza vitu kama hivi visivyoofaa! (**Talking as he moves towards his car**) Sawa basi, hizo taa zako zichukuwe mwenyewe, nitakwenda agiza zangu mahali pengine...

**28. SFX: LAMPS BEING MOVED APART. SOUND OF STEPS GOING AWAY**

**29. PAPA WALI: (Calls Mr Tô)** Tafadhali Bwana Tô rudi!

Nitarekebisha matatizo yaliyopo. Utaniachiaje taa hizi zote nane?

**30. M. TÔ:** (**From a distance**) Naam, nitakuacha nazo. Ukitaka  
zitumie shambani kwenu. Sizichukui ng'o! Hilo nakuhakikishia...

**31. SFX: SOUND OF GATE OPENING AND CLOSING.**  
**CAR STARTS UP.**

**32. PAPA WALI: (Feeling humiliated and very angry) Loo!!**

Hawa watu wanawadharau wenzao kwa kuwa wamesoma au ni kwasababu ya pesa? Mtu amekuja hapa kaagiza bidhaa za bei ya kutupwa, kapunguziwa na kupunguziwa bei na mara leo ghafla anathubutu kunipa kauli za namna hiyo! Watu wana matatizo humu nchini! Kwa kuwa tuna mashine leo, ndiposa unalalamikia kazi yangu? Nenda unakotaka kwenda! Nenda kwa walio na mashine kubwa. Siku moja utagundua kuwa sisi ndiyo waasisi wa kazi hii humu nchini. Watu wasiokuwa na shukrani! (**To Epiphane**) Una shida gani, Epiphane? Utakaa hapo unitumbulie macho tu?

**33. EPIPHANE: Hapana, mzee!****34. PAPA WALI: Basi ziondoe hapa taa hizi! Sitaki kuziona!****35. SFX: SOUND OF STEPS AND THE LAMP BARS  
BEING PUT SOMEWHERE, SIMULTANEOUS FILING  
NOISE...****36. NARRATOR: Papa Wali alishindwa kupata usingizi usiku huo.**

*Mkewe Mamoua ana wasiwasi kwa kuwa mume wake hakuweza kula chakula cha jioni.*

### **Scene 3, AT PAPA WALI'S HOME:**

Papa Wali and Mamoua

**37. ATMO: CRICKETS, NIGHTBIRDS IN THE BACKGROUND, SOUND OF BEDSPRINGS /TURNING IN ONE'S BED**

**38. MAMOUA:** Wali, Mbona hunielezi linalokusumbua?

**39. PAPA WALI: (moans)**

**40. MAMOUA:** Unajua jinsi mke anavyohisi pale mume wake anabaki kugaragara kitandani ilhali mke huyo hajui linalomsumbuu mume wake?

**41. PAPA WALI:** Samahani, Mamoua... Mambo yanatukia kwa wakati mmoja. Madeni, wateja wanakimbia, gharama zinazoongezeka... Asubuhi ya leo, mteja mmoja alinitusi na akakataa kutwaa bidhaa alizokuwa ameagiza eti kwasababu hazikuwa zimetengenezwa vizuri. Na leo jioni, Latifa aliquwa akinisubiri hapa baada ya kufukuzwa shulen i kwa kuwa hajalipiwa karo... kaka yake naye hajalipa kodi ya nyumba kwa miezi kadhaa na sitaki ateseke kwa kulala rafu kwani ningependa ajiunge na chuo kikuu... (**Silence**)

**42. MAMOUA:** (**Sighs**) Wali mume wangu! Maisha ni magumu kote, au sivyo? Kila mtu analalamika kuwa vitu vyote viko ghali. Lakini ilikuwaje mteja hakuvipata alivyoviagiza? Pengine ungetumia fedha hiso kulipa kodi ya Elinam.

**43. PAPA WALI:** Bila shaka siwezi kumtengezea bidhaa sawa na  
hizo zitokazo kiwandani eti. Mimi si mashine!

**44. MAMOUA:** Mbona hukumweleza hayo tangu mwanzo?

**45. PAPA WALI:** Mwanaume gani atasema hawezi kazi aliyopewa?  
Kauli hiyo itakukosesha mteja moja kwa moja.

**46. MAMOUA:** Ndiyo, lakini umemkosa huyo mteja wako kwa  
njia hiyo na wala hajakulipa fedha ulizotumia kumtengenezea bidhaa  
zake. Utalipaje kodi ya mwanao? Suala la Latifa si tatizo. Nadhani  
anapaswa kukoma kusoma. Kuna haja gani ya kumsomesha  
msichana ambaye ataishia jikoni kwa mwanamume akimpikia tu?

**47. PAPA WALI:** Sijui ... Kama hilo ndilo lingekuwa tatizo pekee...

**48. MAMOUA:** Wali, safari ndefu huanzia na hatua ya kwanza na  
hapa tuanze na ile isiyotatiza sana. Hayo mengine tutaenda nayo  
hatua kwa hatua.

**49. PAPA WALI:** Nadhani uko sahihi. Itanibidi nimalize hasira  
ndipo tuipate suluhu.

**50. MAMOUA:** Sawa kabisa Mume wangu. Jitulize upate usingizi  
angalau. Jaribu....

**51. PAPA WALI:** Sawa mke wangu... Alamsiki!

**52. ATMO: TURNING IN BED, RUSTLE OF CLOTHES,  
SOFT MUSIC + INSECTS + NIGHTBIRDS**

**53. NARRATOR:** *Kesho yake, alfajiri kabla majogoo kuwika, Mamoua alimuamsha binti yake Latifa kwani alikuwa na mazungumzo naye. Latifa aliketi kitako kwenye kisiki akimsilikiza mamake ila alichanganywa na kauli zake.*

**Scene 4, AT PAPA WALI'S HOME:**

Mamoua and Latifa

**54. SFX ATMO: COCK CROWING, SOUND OF POTS AND  
PANS BEING WASHED AND PUT AWAY, YARD BEING  
SWEPT...**

**55. MAMOUA:** Nisikize kwa makini, Latifa. Mimi ni mamako. Ninakutakia mema tu katika maisha yako ya baadaye. Unajua kuwa babako sasa hivi ana matatizo chungu nzima na inatubidi tumsaidie kuyatatua. Elimu yako imekuwa ghali sana kwake wala siwezi kufidia gharama hizo na pato la biashara ya uji. Unaweza kusoma, unaweza kuandika. Msichana anahitaji nini cha ziada shulen? Inakubidi uache masomo binti yangu.

**56. LATIFA:** Lakini Mama, ninatakikana kufanya mitihani mwaka huu na inanibidi niipite ili nipate cheti changu cha kwanza cha masomo. Imesalia miezi sita tu mpaka hapo tutakapofanya mitihani.

**57. MAMOUA:** Latifa, wewe ndiwe unayelipa karo?

Nimeshakwambia kwamba hatuwezi tena. Kaka yako yuko chuo kikuu na hatuwezi hata kulipa kodi yake. Ungependa aishie barabarani badala ya kurejea nyumbani akiwa amehitim shahada yake?

**58. LATIFA:** (**Pleading voice**) Na mimi ndiye niache shule?

Kulikuwa na haja gain ya kuyaanza ikiwa hapana haja ya kupata hata cheti cha kiwango cha chini ingawa sijawahi kuanguka mtihani wowote? (**Bursts into tears**) Vipi Jaurès ambaye kila mwaka inambidi kurudia darasa? Mbona asiache masomo?

**59. MAMOUA:** Unapaswa kumsaidia mdogo wako badala ya kauli za aina hiyo.Jaurès ni mvulana na siku moja itambidi aanze mji wake na atafute riziki.Wewe ni msichana. Hata ufaulu vipi, mwisho wako utakuwa mama wa nyumbani. Ikiwa hutapata mtu akupe ujauzito kabla...

**60. LATIFA:(Still in tears)** Kwanini unaniambia mambo haya mabaya, mama? Uliwahi kuniona lini na mvulana? (**Very annoyed**) Wewe ndiwe unayefikiria kwamba mwanamke anapaswa kumtegemea mwanaume, si mimi. Sitaki kuishia kama wewe kamwe!

**61. MAMOUA:** Alaa! Unajua nini wewe?

**62. LATIFA:(Very firmly)** Ninachojua ni kwamba lazima nirejee

shuleni, ili nifanye kazi na kufidia gharama zangu.

**63. MAMOUA:** (Shouting) Rejea basi! Uza nguo zako ujilipie

karo! (**Latifa goes off and her mother shouts after her**) Hivi

unaondoka? Mwangalie, wasichana wa siku hizi mna mambo. Wakati

wetu hatungethubutu kujibizana na wazazi. Mnajifunza nini huko

shuleni? Mnafunzwa jinsi ya kukosa adabu pia?

**64. SFX ATMO HENS + SHEEP + BIRDS**

### Music

#### **OUTRO:**

*Hatma ya Latifa imeingia doa. Jee msichana huyu mwerevu ataishia kukaa nyumbani? Atawezaje kukabiliana na shinikizo la wazazi peke yake? Papa Wali na mkewe Mamou watafanikiwa kuyasuluuhisha matatizo yao? Ili ufahamu zaidi, usikose kusikiliza kipindi kitakacholeta cha “Mtoto wa kike amaliza masomo”, mfululizo wa vipindi kuhusu elimu na kutojua kusoma na kuandika uliotayarishwa na Frédéric Gakpara.*

**Ukitaka kusikiliza vipindi vyote vya mfululizo wa Learning by Ear ambavyo tayari vimeshapeperushwa hewani na idhaa ya Deutsche Welle, tazama ukurasa wetu wa tovuti [www.dw-world.de/lbe](http://www.dw-world.de/lbe).**

**Unaweza pia kutuandikia barua-pepe kupitia anwani: [lbe@dw-world.de](mailto:lbe@dw-world.de) Tunakushukuruni nyote mliotusikiliza. Kila la heri hadi mara nyingine tutakapokutana!**

**END OF 1<sup>ST</sup> EPISODE**

